

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA SITINI

28 JUNI, 2018



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA SITINI – TAREHE 28 JUNI, 2018

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Hati ya Uhamishaji Fedha Na. 1 ya Mwaka 2017/2018
(*Statement of Reallocation Warrant No. 1 of 2017/2018*).

Hati ya Uhamishaji Fedha Na. 2 ya Mwaka 2017/2018
(*Statement of Reallocation Warrant No. 2 of 2017/2018*).

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

505. MHESHIMIWA ZACHARIA PAUL ISSAAY (MBULU MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hali ya barabara zinazosimamiwa na Halmashauri ni mbaya sana kutokana na fedha zinazotolewa na mfuko wa barabara kukaa kwa muda mrefu na hali ya kuongezeka kwa magari binafsi na yale ya biashara ambapo kila Taraifa ina zaidi ya magari 20 na hivyo kufanya barabara hizo kuharibika na kuwa vigumu kupidika nyakati za masika:-

- (a) Je, Serikali haioni haja ya kuleta mapendekezo mapya ya mgao wa fedha za barabara;
- (b) Barabara nyingi za Halmashauri ya Mji wa Mbulu zimejifunga katika Taraifa za Nambis na Daudi; Je, kwa nini Wataalam toka Wizarani wasifike kuzikagua na kutoa ushauri stahili;
- (c) Je, kwa nini BQ za tenda za barabara ngazi ya Mkoa zisiwekwe kwenye kitabu cha RRB ili Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wafahamu shughuli zitakazofanywa na Makandarasi waliopewa kazi.

506. MHESHIMIWA JOEL MWAKA MAKANYAGA (CHILONWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Barabara inayounganisha Kata ya Haneti na Kata ya Segala kuitia Kata ya Zajilwa ni muhimu sana kwa kufungua mawasiliano katika Kata hizo tatu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa barabara hiyo inatengenezwa kwa kiwango cha kuitika muda wote kwa mwaka.

WIZARA YA MADINI:

507. MHESHIMIWA DKT. DALALY PETER KAFUMU (IGUNGA):

Atamuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:- Wawekezaji wanaotaka kuja kuwekeza kwenye Sekta ya Nishati na Madini wamepungua sana katika kipindi cha miaka mitano iliyopita:-

(a) Je, ni nini kimesababisha hali hiyo;

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kuwa Wawekezaji wanaendelea kuja ili kukuza uwekezaji kutoka nje [Foreign Direct Investment (FDI)].

WIZARA YA KILIMO:

508. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Tumbaku inayolimwa Mkoani Tabora inachangia pato kubwa la Taifa:-

Je, Serikali ipo tayari kuboresha mazingira ya kilimo hicho ili kisiathiri mazingira.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

509. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Kesi za dawa za kulevyta na upelelezi vimekuwa vikichukua muda mrefu sana na kusababisha wakati mwingine ushahidi kupotea na Watuhumiwa kuachwa huru baada ya upelelezi kukamilika:-

Je, kwa nini Serikali isianzishe Mahakama za Dawa za Kulevyta kwenye Viwanja vya Ndege, Bandari na mipakani ili Watuhumiwa wafikishwe Mahakamani punde tu ushahidi ukiwa mikononi kama zifanyavyo nchi nyingine ikiwemo India.


IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na
Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada ya Sheria ya Fedha wa Mwaka 2018 (The Finance Bill, 2018).

DODOMA
28 JUNI, 2018

S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE



BUNGE LA TANZANIA